# HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA

## MUHTASARI WA KIKAO CHA KAWAIDA CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO KILICHOFANYIKA TAREHE 22/10/2021 KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI.

### WAJUMBE WALIOHUDHURIA

| | | |
|---|---|---|
| 1. Mh. Duncan B. Urassa | Diwani Kata ya Karansi | **Mwenyekiti** |
| 2. Mh. Noel P. Mollel | Diwani Kata ya Ormelili | Mjumbe |
| 3. Mh. Jane C. Kimaro | Diwani Viti Maalum | Mjumbe |
| 4. Mh. Tawida N. Basso | Diwani Viti Maalum | Mjumbe |
| 5. Mh. Zacharia L. Lukumay | Diwani Kata ya Gararagua | Mjumbe |
| 6. Mh. Patrick J. Kimario | Diwani Kata ya Ngarenairobi | Mjumbe |
| 7. Mh. Nsonuu Lwite Ndossi | Diwani Kata ya Donyomurwa | Mjumbe |

### WAJUMBE WASIOHUDHURIA - KWA TAARIFA

| | | |
|---|---|---|
| 1. Mh. Dkt. Godwin O. Mollel | Mbunge wa Jimbo la Siha | Mjumbe |

### WATAALAM WALIOHUDHURIA

| | |
|---|---|
| 1. Ndg. Mangali. U.E | Mkurugenzi Mtendaji Wilaya **Katibu** |
| 2. Ndg. Constantine M.Mtiti | Mkuu wa Idara ya Mipango,Takwimu na Ufuatiliaji |
| 3. Ndg. Mathias Maskini | Kaimu Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira |
| 4. Ndg. Habibu Ally | Mkuu wa Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika |
| 5. Ndg. Zakayo E. Mosha | Mkuu wa Kitengo cha Habari na Mawasiliano |
| 6. Ndg. Angela F. Kilawe | Mkuu wa Kitengo cha Uchaguzi |
| 7. Ndg. Neema Aligawesa | Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala |
| 8. Ndg. Conjesta Pastory | Kaimu Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi |
| 9. Ndg. Biliard Mrindoko | Kaimu Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara |
| 10. Ndg. Lazaro Mwaluko | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Nyuki |
| 11. Ndg. Alfred R. Mwitumba | Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi na Zimamoto |
| 12. Ndg. Annastazia Mahoo | Afisa Ushirika |
| 13. Ndg. Suleiman Mpanju | Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi na Ugavi |
| 14. Ndg. Madangi J. Bura | Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi |
| 15. Ndg. Frank Mbaga | Kny. Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani. |
| 16. Ndg. Marco Masue | Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii |
| 17. Dkt. Peter Mahu | Mkuu wa Idara ya Afya |
| 18. Ndg. Agrey Kyando | Mtakwimu |
| 19. Ndg. Elizabeth Pagama | Afisa Biashara |
| 20. Ndg. Ansila Muneth | Afisa Utumishi |
| 21. Ndg. Mbaraka Kiure | Fundi Sanifu Ujenzi |
| 22. Ndg. Andrea Biashara | Afisa Mipango Miji |

### SEKRETARIETI

| | |
|---|---|
| 1. Ndg Tupilike Asukile | Mwandishi wa vikao |
| 2. Ndg. Elineema Mmari | Mwandishi wa Vikao |
| 3. Ndg. Ninael R. Maimu | Katibu Mahususi |

**MUHT 201/10/2021 KUFUNGUA KIKAO.**
Katibu alimkaribisha Mwenyekiti kufungua kikao. Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe na wataalam kwenye kikao. Mwenyekiti alifungua kikao saa 3:53 asubuhi baada ya sala.

**MUHT NA 202/10/2021 KURIDHIA AGENDA**
Katibu alisoma agenda za kikao na wajumbe waliridhia kama ifuatavyo:-

1. Kufungua kikao.
2. Kuridhia Agenda.
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao kilichopita cha tarehe 22/09/2021
4. Yatokanayo na muhtasari wa kikao cha tarehe 22/09/2021.
5. Taarifa ya Mapato na Matumizi Mwezi Septemba, 2021
6. Taarifa ya mapokezi ya fedha, Mwezi Septemba, 2021
7. Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kipindi cha Julai hadi Septemba, 2021.
8. Taarifa za Utekelezaji kazi za Idara robo ya kwanza, Julai hadi Septemba, 2021 na mpango kazi robo ya pili, Oktoba hadi Desemba, 2021.
    a. Idara ya Utumishi na Utawala
    b. Kitengo cha Uchaguzi
    c. Kitengo cha Habari na Mawasiliano
    d. Kitengo cha Sheria
    e. Kitengo cha ugavi na manunuzi
9. Mpango wa Masomo kwa watumishi kwa mwaka 2021/2022
10. Taarifa ya Mpango wa Maendeleo ya Ustawi na Mapambano dhini ya Uviko- 19.
11. Taarifa ya kufanya uhamisho wa vifungu katika fedha za Miradi ya Maendeleo.
12. Kupitisha mikopo kwa vikundi vilivyoomba
13. Taarifa mbalimbali.
14. Kufunga kikao.

**MUHT NA. 203/10/2021 KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 22/09/2021**
Wajumbe walipitia muhtasari ukurasa kwa ukurasa na kuridhia kuwa kumbukumbu za Halmashauri.

**MUHT NA. 204/10/2021 YATOKANAYO NA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 22/09/2021**
Wajumbe walipokea utekelezaji wa maazimio ya kikao kilichopita kama ifuatavyo:-

**132/02/2021(I) OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI IENDELEE KUFUATILIA MAOMBI YA KUPEWA SHAMBA LA LERONGO WIZARA YA KILIMO.**
Wajumbe walipokea utekelezaji kuwa, barua yenye Kumb Na SDC/C.40/1/VI/68 ya tarehe 15/09/2021 imeandikwa kwa Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo kukumbushia maombi ya kupewa shamba la Lerongo. Aidha nakala ya barua hizo amepewa Mhe. Mbunge na Naibu Waziri wa Afya ili asaidie kufuatilia. Pia Mkuu wa Idara ya Kilimo alikutana na Mkurugenzi wa Maendeleo ya Kilimo tarehe 16/09/2021 Jijini Dodoma na kukiri kupokea barua za

Halmashauri ya Wilaya ya Siha za maombi ya shamba hilo na kuahidi kuzifanyia kazi na kutoa majibu kwa haraka. Wajumbe walisema kuwa Mhe. Mbunge bado hajapata barua hiyo, hivyo waliagiza ufuatiliaji uendelee na Mhe. Mbunge apewe barua nyingine kwa ajili ya ufuatiliaji.

**AZIMIO**

Ufuatiliaji wa shamba la Lerongo uendelee Mhe. Mbunge apewe barua nyingine kwa ajili ya kusaidia kufuatilia.

**MUHT NA 138/3/2021(I) TIMU ILIYOUNDWA KWA AJILI YA KUANDAA TAARIFA YA KUANZISHA KITUO CHA UTALII WILAYA YA SIHA IKAMILISHE TAARIFA NA MATANGAZO YATOLEWE KUPITIA MITANDAO YA KIJAMII.**

Wajumbe walipokea utekelezaji kuwa, timu ya kuandaa taarifa ya kuanzisha kituo cha Utalii itakapokamilisha taarifa baada ya kufanya utafiti na kutembelea vivutio vingine kwa ajili ya kujifunza na kupata uzoefu kwa wadau mbalimbali wanaojishughulisha na mambo ya utalii na baada ya hapo ndipo matangazo yatatolewa kupitia mitandao ya kijamii.

Wajumbe walisema kuwa, kazi ya kufanya utafiti ikamilike ndani ya mwezi mmoja tangu siku ya kikao na taarifa iwasilishwe kwenye kikao.

**AZIMIO**

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) ikamilishe kazi ya utafiti wa kuanzisha kituo cha Utalii Wilaya ya Siha ndani ya mwezi mmoja tangu siku ya kikao taarifa iwasilishwe kwenye kikao.

**MUHT NA 158/5/2021 (III) HALMASHAURI IHAKIKISHE IMESAJILI BAJAJI NA KUANZA KUKUSANYA USHURU WA BAJAJI.**

Wajumbe walipokea utekelezaji kuwa, zoezi lilianza tarehe **30/09/2021** kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi ambapo baada ya kuzikamata baadhi ya bajaji, hatimaye wafanyabiashara wa vyombo vya usafirishaji wameanza kujitokeza ambapo hadi sasa jumla ya **bajaji 7 (4 za Sanya Juu na 3 za Lawate)** wamepewa namba dhibiti (control namba) na wamekwishalipia jumla ya **Shs 154,000/=** zilipatikana ambapo kiasi hicho hupelekwa katika mamlaka ya udhibiti usafiri ardhini **(LATRA)** na wao kuturudishia nusu ya makusanyo kwa kila robo.

Idara inaendelea na ufuatiliaji na uhamasishaji wa kina ili kukusanya ada ya Leseni ya usafirishaji kwa wafanyabiashara wote. Wajumbe walisema kuwa, ufuatiliaji unasuasua hivyo Afisa Biashara aongeze kasi bajaji zote zisajiliwe. Aidha mjumbe mmoja alisema kuwa, Hotel ya Osigilai hakuna mapato yanayokusanywa alitaka kufahamu nini mpango wa Halmashauri wa kukusanya mapato hayo. Jibu lilitolewa ufuatiliaji ulifanyika ambapo vitabu vilipelekwa baada ya kuwapa vitabu walisema hawawezi kulipa "hotel levy" kwa sababu wanalipa TALA hivyo kama ni kweli wanalipa TALA Halmashauri haitaweza kutoza ushuru huo. Kutokana na maelezo hayo, wajumbe walisema kuwa Ofisi ifuatilie ili kujiridhisha kisheria kodi ambazo Halmashauri wanaweza kukusanya katika hotel hiyo.

**AZIMIO**

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ifuatilie ili kujiridhisha kisheria kodi ambazo Halmashauri inaweza kukusanya katika hotel ya Osigilai.

**MUHT NA 158/5/2021 (II) UNUNUZI WA TAA ZA SOLAR KWA AJILI YA KUWEKA STENDI YA KIA UHARAKISHWE NA TAA HIZO ZIFUNGWE MAPEMA IWEZEKANAVYO.**

Wajumbe walipokea utekelezaji kuwa, kiasi cha Tshs 3,150, 000/= kimetengwa na taa hizo zitafungwa ndani ya robo ya pili 2021.

Mjumbe alitaka kujua kiasi hicho ni kwa ajili ya taa ngapi. Jibu lilitolewa kuwa ni kwa ajili ya taa tisa, kwa sababu nguzo zilizopo ni tisa. Aidha wajumbe walisema kuwa mapato yameshuka katika stendi ya KIA walitaka kujua hatua iliyofikiwa kwa ajili ya kurekebisha kwani mpaka sasa bararabara ya kuzunguka magari imefungwa kwa mawe kwa sababu wafanyabiashara wanalalamika magari yakipita mengi kwa wakati mmoja yanaacha vumbi. Mjumbe alijibiwa kuwa, suala hilo linafuatiliwa changamoto ni mzabuni wa kufanya kazi alipatikana kwa gharama ya Shs 12 milioni taratibu za manunuzi kutoa fedha zilifanyika mara wakapokea taarifa mzabuni huyo hataweza kufanya kazi kwani magari yake yamepata kazi sehemu nyingine hivyo alisema atachelewesha kazi na kushauri atafutwe mzabuni mwingine.

Baada ya kupokea taarifa hiyo utaratibu wa kutafuta mtu mwingine umefanyika ambapo nukuu za bei zilifanyika na kupata mtu atakayefanya kazi hiyo kwa gharama ya Shs 18 milioni bila VAT ikiwa na VAT itakuwa Shs 21 milioni . Wajumbe walisema kuwa, stendi ya KIA ni chanzo kizuri cha mapato kisicho na msimu hivyo kuchelewa kurekebisha stendi hiyo fedha nyingi zinapotea. Aidha, kwa kuwa mchakato wa kumpata mtu atakayefanya kazi hiyo pamoja na kupatikana kwa fedha umeanza upya, Ofisi ya Mkurugenzi itoe fedha haraka taarifa ya utekelezaji kuhusu kurekebisha stendi ya KIA iwasilishwe kwenye kikao ili kunusuru mapato yanayopotea.

**AZIMIO**

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya iwasilishe taarifa ya utekelezaji kuhusu kurekebisha Stendi ya KIA ili kunusuru mapato yanayopotea.

**MUHT NA 158/5/2021 (III) MENEJIMENTI IFANYE KIKAO CHA KUJADILI NA KUWEKA MPANGO WA KUJENGA VIBANDA STENDI YA KIA NA MPANGO HUO KUWASILISHWA KWENYE KIKAO**

Wajumbe walipokea utekelezaji kuwa, kwa mwaka wa Fedha 2021/2022 Halmashauri imetenga kiasi cha Shs 20,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa vibanda 6 vya biashara katika Stendi ya KIA. Utekelezaji utafanyika robo ya pili ya mwaka wa fedha 2021/2022 Wajumbe walisema kuwa robo ya pili imeanza walitaka kujua utekelezaji umefikia wapi. Mjumbe alijibiwa kuwa, wakati wanatoa jibu hilo Ofisi ilikuwa bado haijapokea maelekezo mengine kuhusu kurudi kwa miradi mikakati.

Halmashauri katika vikao tofauti kipindi cha nyuma iliwahi kujadili eneo la KIA kuwa na mradi mkakati na mtaalam alikuja kuonyesha namna patakavyokuwa baadae maelekezo yakatolewa na Serikali kuwa miradi mikakati isitishwe kwanza. Alisema kuwa sasa Ofisi imepokea maelekezo kuwa miradi mikakati imerudi Ofisi inajipanga tena kwa ajili ya kutafuta mtaalam wa kufanya upembuzi yakinifu baada ya hapo hatua zingine zitafuata ikiwa ni pamoja na kuandaa andiko la mradi. Wajumbe walisema kuwa, kwa kuwa miradi mikakati imerudi ni vyema kusitisha kujenga vibanda ili kukwepa hasara ya kubomoa vibanda, Halmashauri ichangamkie fursa hiyo ili kuwa na chanzo chenye tija. Ushauri ulipokelewa.

**158/5/2021 (IV) HALMASHAURI INUNUE TANKI LA MAJI KWA AJILI YA CHOO CHA STENDI YA KIA KUHIFADHI MAJI ILI YAWEZE KUTUMIKA KWA MATUMIZI YA CHOO PINDI MAJI YANAPOKATIKA.**

Wajumbe walipokea utekelezaji kuwa, Utekelezaji utawasilishwa robo ya pili 2021/2022 Wajumbe walishauri kuwa ununuzi wa tank la maji sio gharama kubwa hivyo linunuliwe.

**MUHT NA 180/7/2021(III) OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI IENDELEE KUFUATILIA UJENZI WA BWAWA LA OROMWI NA TAARIFA YA HATUA ILIYOFIKIWA KATIKA UJENZI HUO IWASILISHWE KWENYE KIKAO.**

Wajumbe walipokea utekelezaji kuwa, ujenzi wa Bwawa bado umesimama kutokana na kuisha kwa fedha za ujenzi. Aidha, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imeahidi kutafuta fedha za kukamilisha ujenzi wa Bwawa hilo. Pia taarifa ya kukwama kwa ujenzi wa bwawa hilo amekabidhiwa Mhe. Mbunge tarehe 29/09/2021 ili asaidie kufuatilia. Aidha Katibu aliwaeleza wajumbe kuwa, majibu hayo yalikuwa ya kipindi cha nyuma walisema fedha zimeisha lakini kwa sasa Ofisi imepokea maelezo kuwa fedha zimepatikana hivyo mafundi watarudi eneo la ujenzi ili kuendelea na kazi. Ushauri ulitolewa kuwa, kwa kuwa fedha zimepatikana kazi ianze mara moja kwa sababu mvua ikinyesha kazi haitaweza kuendelea.

**MUHT NA 180/7/2021 (IV) TAARIFA YA FEDHA ZINAZOHITAJIKA KUKAMILISHA UJENZI WA WODI 2 ZINAZOJENGWA HOSPITALI YA WILAYA IWASILISHWE KWENYE KIKAO.**

Wajumbe walipokea utekelezaji kuwa, vifaa Tshs. 76,941,200/= deni la fundi 12,000,000/= jumla ni Tshs. 88,941, 200/= kwa jengo moja hivyo kwa majengo yote mawili itagharimu kiasi cha Tshs. 177,882,400/= wajumbe walisema kuwa, wataalam wajiridhishe na makisio wanayofanya ili kuwa na uhalisia. Aidha waliagiza taarifa ya mchanganuo wa Tshs 177,882,400/= uwasilishwe kwenye kikao kijacho. Pia walishukuru Serikali kurudisha fedha Shs. 291 milioni zilizokuwa zimechukuliwa na Hazina baada ya mwaka wa fedha 2019/2020 kufungwa ambazo sasa zitatumika kujenga wodi ya 3. Walisema kuwa, wataalam wawe makini wakati wa kuanza ujenzi wa wodi ya 3 ikiwa ni pamoja na kukagua eneo lisawazishwe ili lisitumie fedha nyingi. Pia vifaa vinunuliwe vinavyohitajika pekee na ufuatiliaji wa hatua kwa hatua uwepo ili vifaa vilivyoagizwa viweze kutosha.

**AZIMIO**

Taarifa ya mchanganuo wa Shs 177,882,400/= kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa wodi mbili Hospitali ya Wilaya uwasilishwe kwenye kikao ikionyesha mchanganuo wa ununuzi wa vifaa.

**MUHT NA 187/8/2021 TAARIFA YA KINA YA MAPATO NA MATUMIZI YA KIWANDA CHA TOFALI NA MBAO PAMOJA NA TAARIFA YA VIFAA VYOTE VYA UJENZI VILIVYONUNULIWA KUTOKA KWENYE VIWANDA MBALIMBALI IWASILISHWE KWENYE KIKAO.**

Wajumbe walipokea taarifa na kuipitia ukurasa kwa ukurasa. Aidha wajumbe walisema kuwa taarifa imeandaliwa na kuweka gharama kwa mafungu hivyo taarifa haijawa wazi ili kupunguza maswali yasiyo ya lazima. Alisema kuwa, mfano saruji taarifa ingeonyesha vifaa vilivyonunuliwa vimeleta faida kiasi gani na wameokoa kiasi gani. Pia uhakiki wa kina ufanyike kujua mchanga ujazo gani unatoa tofali ngapi sambamba na kujua mfuko wa saruji unatoa tofali ngapi. Aidha, kwa upande wa mbao taarifa imeandikwa kwa jumla hivyo kuelewa ni vigumu mbao ya "size" gani iliyopigiwa hesabu. Waliomba taarifa iwasilishwe ikiwa na mchanganuo ili kurahisisha kuelewa. Pia wajumbe walitaka kujua kama mradi wa kiwanda cha tofali na mbao unaendelea.

Akijibu hoja hiyo, katibu alieleza kuwa, kwa upande wa kiwanda cha tofali na mbao kutokana na mifumo ya fedha kufungwa baadhi ya kazi zilisimama lakini zingine za umaliziaji ziliendelea kufanyika. Mpango wa kuagiza vifaa vingine unaandaliwa ili kuendelea kuzalisha. Aidha wajumbe walishauri kuanzisha kampuni ili mradi huo uwe na tija zaidi. Katibu alijibu kuwa, kuanzisha kampuni ni sawa lakini alitoa angalizo kwa wajumbe kuwa wangetafakari kwanza kwa kina kwa sababu kiwanda hakijamaliza hata miaka miwili ili waone kama kina tija au hapana. Hata hivyo Katibu alijibu kuwa, ushauri umezingatiwa watafanyia kazi.

**MAAZIMIO**

I. Taarifa ya kiwanda cha tofali na mbao iwasilishwe kwenye kikao ikiwa na mchanganuo wa mbao kila size, idadi na mita zake.
II. Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji iagize vifaa vingine kiwanda cha tofali na mbao kiendelee kuzalisha.

**MUHT NA 197/9/2021(I) OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI ITOE TAARIFA KWENYE KIKAO KIJACHO KUHUSU MATENGENEZO YA KIFAA KILICHOHARIBIKA KWENYE MFUMO WA KUTOA RISITI.**

Wajumbe walipokea utekelezaji kuwa, mashine imerekebishwa risiti zimeanza kutolewa. Wajumbe waliridhia utekelezaji.

**MUHT NA 197/9/2021(II) OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA IENDELEE KUFUATILIA NA KUHAKIKISHA KUWA WAKULIMA HAWAPUNJWI WANAPOUZA MAZAO YAO NA KUZUIA WAFANYABIASHARA WANAONUNUA MAZAO YA WAKULIMA NJE YA MFUMO RASMI.**

Wajumbe walipokea utekelezaji kuwa, barua yenye kumb na SDC/A.30/3/VII/30 ya tarehe 15/08/2021 imeandikwa kwa Watendaji wa Vijiji vyote kusimamia udhibiti wa ufungashaji na vipimo vya uuzaji wa mazao visivyo sahihi. Aidha matangazo yameandikwa maeneo mbalimbali pamoja na kutumia gari la matangazo kuwatangazia wakulima na wananchi

kuwataka kutumia vipimo sahihi vya mazao. Wajumbe waliridhia utekelezaji na kushauri ufuatiliaji uendelee ili wakulima wasiibiwe.

**MUHT NA 199/9/2021 TAARIFA YA KUANZA UJENZI WA KITUO CHA AFYA KATA YA OLKOLILI IWASILISHWE KWENYE KIKAO IKIONYESHA HATUA ILIYOFIKIWA KATIKA UJENZI HUO.**

Wajumbe walipokea taarifa na kuagiza Ofisi iendelee kufuatilia ujenzi huo taarifa ya hatua iliyofikiwa iwasilishwe kwenye kikao.

**AZIMIO**

Taarifa ya ujenzi wa kituo cha Afya Kata ya Olkolili iwasilishwe kwenye kikao ikionyesha hatua iliyofikiwa.

**MUHT NA 205/10/2021 TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI MWEZI SEPTEMBA 2021.**

Kaimu Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara aliwasilisha taarifa kuwa, kwa mwaka wa fedha **2021/2022** Halmashauri ya Siha imekisia kukusanya na kupokea kiasi cha Shs. **21,440,691,272.67** kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato ya ndani, ruzuku toka Serikali Kuu na Wahisani kwa ajili ya matumizi ya kawaida, mishahara na utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Aidha kiasi cha Shs 162,309,962 ni bakaa ya mwaka 2020/2021 na kufanya jumla ya makisio kuwa Shs **21,603,001,234.67**

Kwa upande wa matumizi ya kawaida, Mishahara na Miradi ya Maendeleo kiasi kilichokadiriwa kutumika ni sawa na kiasi kinachotarajiwa kupokelewa na kukusanywa cha **Shs. 21,440,691,272.67** ikiwa ni makisio ya mapato ya mwaka 2021/2022 na Bakaa kiasi cha **Shs. 162,307,962** sawa na jumla ya Shs. **21,603,001,234.67**

**MAPATO**

Katika kipindi cha mwezi Septemba, 2021 Halmashauri imepokea na kukusanya kiasi cha **Shs. 1,260,406,888.68** kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato ya ndani, ruzuku toka Serikali Kuu na Wahisani. Aidha mapato pamoja na bakaa hadi mwezi Septemba, 2021 kuwa jumla ya **Shs 4,112,567,507.09** sawa na asilimia **19.04** ya lengo la makisio ya mapato kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**MATUMIZI.**

Kwa kipindi cha mwezi Septemba, 2021 Halmashauri imetumia kiasi cha **Shs.1,289,302,732.49** katika kulipa mishahara ya watumishi, matumizi ya kawaida na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Aidha matumizi yote kuanzia mwezi Julai hadi Septemba, 2021 pamoja na Bakaa kufikia **Shs 3,530,228,421.08** sawa na asilimia 16.34 ya lengo la matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Wajumbe walipokea taarifa na kuanza kujadili. Mjumbe mmoja alisema kuwa, kwa ujumla mapato yamekusanywa kwa asilimia 16 pekee aliomba nguvu ya kukusanya iongezwe ikiwa ni pamoja na kuweka nguvu zaidi kuboresha Stendi ya KIA kwani mapato yake ni ya uhakika, pamoja na kukusanya ushuru wa Vibanda na usajili wa bajaji.

**MUHT 206/10/2021 TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA MWEZI SEPTEMBA, 2021.**
Kaimu Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara aliwasilisha taarifa ya mapokezi ya fedha kwa mwezi septemba, 2021 yenye jumla ya **Shs 1,180,180,033.80**
Wajumbe walipokea taarifa na kuridhia.

**MUHT 207/10/2021 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KIPINDI CHA JULAI HADI SEPTEMBA, 2021**
Katibu aliwasilisha taarifa kwa kueleza kuwa, mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri ilikadiria kupokea kiasi cha **Shs 6, 610,511,511,293.00** za miradi ya maendeleo kutoka mapato ya ndani ya Halmashauri, Ruzuku kutoka Serikali Kuu na wadau wa Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Septemba, 2021 Halmashauri imepokea kiasi cha Shs. 786,409,388.00 sawa na asilimia 12 ya fedha za miradi ya maendeleo zilizokusudiwa kupokelewa kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Hadi kufikia mwezi Septemba, 2021 Halmashauri imetumia kiasi cha **Shs. 481,236,661.00** ikiwa ni pamoja na fedha za bakaa ya mwaka wa fedha 2020/2021 sawa na asilimia 7 ya makisio ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Wajumbe walipokea taarifa na kuridhia.

**MUHT 208/10/2021 TAARIFA ZA UTEKELEZAJI KAZI ZA IDARA ROBO YA KWANZA, JULAI HADI SEPTEMBA, 2021 NA MPANGO KAZI ROBO YA PILI, OKTOBA HADI DESEMBA, 2021.**
**IDARA YA UTUMISHI NA UTAWALA**
Katibu aliwasilisha taarifa ya utekekezaji Idara ya Utawala kwa kueleza kuwa, robo ya kwanza Idara iliidhinishiwa kiasi cha Shs 47,505,000.00 na ilitumia kiasi cha **shs 25,291,000.00**. Aidha robo ya pili kipindi cha Oktoba hadi Desemba, 2021 Idara inatarajia kutumia kiasi cha **Shs 40,549,535.25.**
Wajumbe walipokea taarifa na kupitisha.

**Kitengo cha Uchaguzi**
Katibu aliwasilisha taarifa kwa kueleza kuwa, robo ya kwanza Julai hadi Septemba 2021 Kitengo hakijatumia fedha yoyote. Aidha katika robo ya pili Oktoba hadi Desemba,2021 Kitengo kinatarajia kutumia kiasi cha **Shs 17,699,000/=** Wajumbe walipokea taarifa na kujadili. Mjumbe mmoja alisema kuwa, ni muda sasa wametoa taarifa ya baadhi ya Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji kujiuzulu hivyo katika maeneo mbalimbali hakuna viongozi jambo ambalo linasababisha kuchelewa kwa shughuli za maendeleo. Alitaka kufahamu ni lini uchaguzi utafanyika ili kuziba nafasi wazi. Akijibu hoja hiyo Mkuu wa Kitengo cha Uchaguzi kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya alieleza kuwa, uchaguzi wa Viongozi hao utafanyika mwezi Januari baada ya kufanyika "reallocation" mwezi Desemba, 2021 kwa ajili ya fedha za kuendesha zoezi hilo. Wajumbe walisema kuwa, utekelezaji ufanyike kwa sababu hata michango ya miradi ya maendeleo haikusanywi ipasavyo kutokana na ukosefu wa viongozi hao. Ushauri ulipokelewa.

**Kitengo cha Habari na Mawasiliano**
Katibu aliwasilisha taarifa kwa kueleza kuwa, kipindi cha Julai hadi Septemba, 2021 Kitengo kiliidhinishiwa kutumia kiasi cha Shs 2,050,000/=. Aidha robo ya pili Oktoba hadi Desemba, 2021 Kitengo kinatarajia kutumia Shs 2,050,000/=.

Wajumbe walipokea taarifa na kuridhia.

**Kitengo cha Sheria**

Katibu aliwasilisha taarifa kwa kueleza kuwa, katika kipindi cha robo ya kwanza Julai hadi Septemba 2021 kitengo kiliidhinishiwa kutumia kiasi cha Shs. 1,800,000/= hakuna fedha iliyopokelewa. Robo ya Pili Oktoba hadi Desemba 2021 Kitengo kinatarajia kutumia kiasi cha Shs. 1,800,000/=. Wajumbe walipokea taarifa na kujadili. Mjumbe mmoja alisema kuwa Kitengo hicho kiwezeshwe ili kiweze kufanya kazi ya kutoa elimu kwa mabaraza ya Kata kwa sababu mabaraza hayo yanatekeleza majukumu yake bila kufahamu mipaka yao. Pia wajumbe walisema kuwa, Mwongozo wa mabaraza ya Kata uwasilishwe kwenye kikao ili wajumbe wafahamu.

**AZIMIO**

I. Kitengo cha Sheria kiwezeshwe kiweze kutekeleza majukumu yake hasa kutoa elimu kwa Mabaraza ya Kata.
II. Mwongozo wa mabaraza ya Kata uwasilishwe kwenye kikao

**Kitengo cha Ugavi na Manunuzi**

Katibu aliwasilisha taarifa kwa kueleza kuwa, kipindi cha Julai hadi Septemba 2021/2022 bidhaa zilizonunuliwa pamoja na huduma mbalimbali zilizotolewa katika Halmashauri zilifikia kiasi cha Tshs 21,002,110.94 ikiwa ni bidhaa mbalimbali na mafuta kwa Idara mbalimbali za Halmashauri pamoja na manunuzi ya ngazi za chini. Mchanganuo ni kama ifuatavyo;

- Manunuzi ya bidhaa, mafuta kwa robo ya kwanza 2021/2022 Makao Makuu yamefanyika yenye Jumla ya Shs. 28,888,323.9
- Manunuzi Elimu Msingi yenye jumla ya Shs. 91,555,227
- Manunuzi ya Elimu Sekondari yenye jumla ya Shs. 4,582,560

Aidha pamoja na manunuzi hayo kufanyika Kitengo kimefanya kazi zingine zifuatazo:-

- Kuratibu kikao cha Bodi ya Zabuni cha robo ya kwanza Julai hadi Septemba, 2021/2022
- Kusimamia na kutoa ushauri wa manunuzi mbalimbali ya Halmashauri ngazi ya Wilaya na ngazi za chini.
- Kuendelea kujibu hoja za ukaguzi zinazojitokeza.

Wajumbe walipokea taarifa na kuridhia.

**MUHT NA 209/10/2021 MPANGO WA MASOMO.**

Wajumbe walipokea taarifa ya mpango wa masomo kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Ilielezwa kuwa, kila Idara baadhi ya watumishi wanatarajia kwenda masomoni kama ifuatavyo:-

Idara ya Maendeleo ya Jamii – 3
Idara ya Kilimo - 4
Idara ya Afya - 9
Idara ya Utawala - 6
Idara ya Mifugo na Uvuvi - 3
Idara ya Fedha - 2
Kitengo cha TEHAMA - 1
Idara ya Mipango - 1
Idara ya Elimu Msingi - 7

Wajumbe walipokea taarifa na kujadili. Mjumbe alitaka kujua endapo wataenda wengi haitaathiri utendaji wa kazi. Jibu lilitolewa kuwa Ofisi inahakikisha imejiridhisha na watumishi watakaobaki hivyo watumishi watakaokwenda masomoni ni wachahe ili kazi zisikwame. Wajumbe waliridhia majibu na kupitisha mpango wa masomo wa mwaka 2021/2022

**MUHT NA 210/10/2021 TAARIFA YA MPANGO WA MAENDELEO YA USTAWI NA MAPAMBANO DHINI YA UVIKO- 19**

Katibu aliwasilisha taarifa kuwa, Halmashauri ya Wilaya ya Siha imeidhinishiwa kupokea **Shs. 1,150,000,000** kutoka fedha za ruzuku ya **Mpango wa maendeleo kwa ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya UVIKO- 19.** Fedha hizi zitatumika kujenga vyumba vya madarasa 18 katika shule 6 zenye upungufu wa madarasa, kujenga vyumba 14 vya madarasa katika vituo 4 shikizi vya shule za msingi, kununua mashine moja ya X-Ray katika Hospitali ya Wilaya na kujenga nyumba moja ya familia tatu wa sekta ya Afya.

**1.0 Ujenzi wa vyumba 18 vya madarasa katika shule za Sekondari.**

Halmashauri ya Wilaya ya Siha imeidhinishiwa kupokea kiasi cha shs. 360,000,000 kwa ajili ya kujenga vyumba 18 vya madarasa. Lengo la Mradi huu ni

- Kuwezesha wanafunzi wote waliomaliza darasa la saba mwaka 2021 na kufaulu kupata nafasi ya kujiunga na kidato cha kwanza mwezi Januari mwaka 2022.
- Kuondoa mrundikano wa wanafunzi madarasani na hivyo kupunguza uwezekano wa kupata maambukizi ya homa kali ya mapafu UVIKO- 19
- Kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

Gharama ya ujenzi wa chumba kimoja cha darasa pamoja na samani ni Shs. 20,000,000. Mchanganuo wa shule na kiasi cha fedha kilichoidhinishwa kwa kila shule ni kama inavyoonesha katika Jedwali na. 1 hapo chini.

**Jedwali na.1 Ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule za sekondari**

| Na. | Jina la shule | Mradi | Idadi | Fedha idhinishwa (shs) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Sikirari | Ujenzi wa vyumba vya madarasa | 3 | 60,000,000 |
| 2 | Magadini | Ujenzi wa chumba cha darasa | 1 | 20,000,000 |
| 3 | Karansi | Ujenzi wa vyumba vya madarasa | 3 | 60,000,000 |
| 4 | Matadi | Ujenzi wa vyumba vya madarasa | 4 | 80,000,000 |
| 5 | Esinyari | Ujenzi wa vyumba vya madarasa | 4 | 80,000,000 |
| 6 | Jitegemee Siha | Ujenzi wa vyumba vya madarasa | 3 | 60,000,000 |
| **Jumla** | | | **18** | **360,000,000** |

Wajumbe walipokea taarifa na kujadili. Mjumbe mmoja alisema kuwa, Kata nyingine hazijapata mkopo ikiwemo Kata ya Gararagua. Jibu lilitolewa kuwa, mkopo umetolewa kwa awamu maeneo yaliyokosa awamu hii yatapata awamu nyingine. Wajumbe walipokea taarifa na kupitisha vikundi hivyo vipatiwe mkopo.

**MUHT NA 213/10/2021 TAARIFA MBALIMBALI**

**Taarifa ya ziara ya kamati ya Fedha Uongozi na Mipango robo ya kwanza Julai hadi Septemba 2021/2022.**

Katibu aliwasilisha taarifa kwa kueleza kuwa, Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango ilifanya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo kuanzia tarehe 20-21/10/2021 ili kujionea na kujiridhisha na kazi inayofanyika kutekeleza miradi hiyo. Miradi iliyotembelewa ni pamoja na:-

1. Ujenzi wa Zahanati Kijiji cha Mwangaza.
2. Ujenzi wa wodi 2 Hospitali ya Wilaya.
3. Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa na Ofisi 1 katika shule ya msingi Mawasiliano.
4. Ujenzi wa mabweni 2 katika shule ya Sekondari Sanya Juu.
5. Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa shule ya Sekondari Dahani.
6. Ujenzi wa madarasa 2 na Ofisi 1 shule ya msingi Namayani.
7. Ujenzi wa matundu 12 ya choo S/Msingi Lekrimuni.
8. Ujenzi wa maabara shule ya Sekondari Esinyari.
9. Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa na Ofisi 1 Shule ya Msingi Olkolili.
10. Ukamilishaji wa vyumba 2 vya madarasa shule ya Sekondari Esinyari.

Wajumbe walisema kuwa, kuna maagizo yalitolewa kuhusu Watendaji ambao hawawajibiki katika kusimamia utekelezaji wa miradi ya Maendeleo. Walitaka kufahamu kama walishaitwa Ofisini kama walivyoagiza. Jibu lilitolewa kuwa, tayari Ofisi imeshawaita na wametoa maelezo.

**Kuvamiwa kwa uwanja wa Isanja**

Ilielezwa kuwa, uwanja huo umekuwa ukivamiwa siku hadi siku hivyo ni wakati wa Halmashauri kuhakikisha wanaweka mawe/bicon kwa ajili mipaka ili wananchi wasisogee kuvamia uwanja huo. Alisema kuwa uwanja huo ni muhimu sana kwani ndio uwanja pekee mkubwa kwa shughuli zinazohusisha watu wengi. Ushauri ulipokelewa.

**MUHT NA 214/10/2021 KUFUNGA KIKAO**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti kufunga kikao. Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe na wataalam kwa kuhudhuria kikao na kujadili agenda kwa kina. Alisisitiza stendi ya KIA ipewe kipaumbele kuikarabati ili magari yaweze kuingia sambamba na kusisitiza kuendelea kufuatilia kwa karibu kiwanda cha tofali na mbao kuhakikisha kazi haisimami na kifanye kazi ili kufikia lengo lililokusudiwa. Alisema kuwa, timu ya mapato iwezeshwe kwa kupewa motisha ili wafanye kazi kwa moyo. Mwenyekiti alifunga kikao saa 9.35 alasiri kwa sala.

**UMETHIBITISHWA**

**KATIBU** **MWENYEKITI**

30/11/2021
...................
**TAREHE**